Kiumbe Kipya Katika Kristo

na

Ellis P. Forsman

Kiumbe Kipya Katika Kristo

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kiumbe Kipya Katika Kristo

2 Kor. 5:17

2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya.*"

Mwanafunzi wa asili ya kibinadamu anahitaji tu kujitazama mwenyewe ili kuona uharibifu na uchafu wa kibinadamu. Anapitia makusudi maovu ya moyo kusababisha aseme na Isaya (Isa. 53:6), "*Sisi sote kama kondoo tumepotea…",* na Paulo (Rum. 3:23), "*Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;"*

Hivyo tunaona kwamba mwanadamu lazima apitie mambo magumu na mabadiliko taratibu kabla hajaitwa Mkristo vizuri. Uhusiano wake kwa Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu lazima ubadilishwe kabla hajavaa kimaandiko jina lenye heshima la Mkristo.

Badiliko hili ni uhamisho kutoka katika ufalme wa Shetani hadi katika ufalme wa Kristo.

Kol. 1:13-14, "*Naye alituokoa katika nguvu za giza akatuamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi yaani msamaha wa dhambi.*"

Yesu anaiita uongofu na kuzaliwa kupya.

- Mathayo 18:3, "*Akasema amini nawaambia, msipoongoka na kuwa kama vitoto hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.*"
- Yohana 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambia, amin, amini, nakuambia mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, amin, amin, nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.*"

Katika kifungu inawakilishwa na kuwa kiumbe kipya.

Ni nini kinachochangia badiliko hili?

Utu wa kale unavuliwa

Efe. 4:22-24, "*Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya; ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*"

Utu wa kale ni nini?

Ile "*Unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya.*"

Utu wa kale unasulubiwa.

Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo lakini ni hai, wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Utu wa kale unazikwa.

- Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

- Kol. 2:12, "*Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu.*"

Je mtu aliyekufa au aliye hai wanaweza kuzikwa katika kifo cha kimwili?

Katika hali ya kiroho ni ipi ambayo tunaweza kuzika?

Paulo anafanya ulinganifu wa maziko ya kitu kimoja na ufufuo wa kingine. Maziko yanahashiria kifo – kuifia dhambi. Ufufuo unahashiria uzima – uzima wa walio haki. Mtu aliyekufa (aliyefia dhambi) hafufuliwi; sawa na mtu aliye hai (aliye hai katika haki) uzikwa.

Kiumbe kipya kinafufuliwa.

Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

Hakuna sehemu ya utu wa kale utakaofufuliwa. Wana wa Mungu ni watakatifu, na wana wa ibilisi ni wachafu. Mwana wa Mungu aliyemchafu atakuwa hana maana sawa na mwana wa ibilisi.

Rum. 6:12, "*Basi dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake.*"

Wengi wanajaribu kuwa viumbe vipya na wanaendelea kushikilia utu wa kale, lakini hiyo tu sio sababu, bali pia ni kinyume na maandiko.

- Isa. 35:8, "*Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia nayo itaitwa, njia ya utakatifu, wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao; wasafirio wajapokuwa wajinga, , hawatapotea katika njia hiyo.*"
- Rum. 12:9, "*Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu mkiambatana na lililo jema.*"
- 1 Kor. 3:16-17, "*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, nay a kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*"
- Ufu. 21:27, "*Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana kondoo.*"

Utu mpya lazima uvaliwe

Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Paulo akasema katika Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Siri ya kiumbe kipya ni kwamba Kristo sasa anaishi ndani ya Paulo. Kupitia muunganiko huu wa ajabu pamoja na Kristo, kiujumla Paulo alikuwa mtu mpya pamoja na mawazo mapya na makusudi.

Kristo sasa anaishi ndani yake kama Mwokozi, mfano, Muongozo, na Mkuu. Vile vile, uongofu katika Kristo haudhofishi uwezo wa wanadamu na kunyausha juhudi zao.

Paulo alikuwa akitenda kazi baada ya kuongoka sawa na jinsi alivyokuwa kabla, lakini hapo nyuma alihusika katika kuwatesa Wakristo; baadaye alitoa talanta zake na nguvu kwa shauku kwa sababu ya Ukristo.

Kwa vile ubatizo ni muhimu ili kuwa kiumbe kipya, je ni nini?

Hebu tuangalie picha iliyowakilishwa katika Biblia:

Maji yanahusishwa.

Mdo. 8:36, "*Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema tazama maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?*"

Maji mengi yalikuwa muhimu.

Yoh. 3:23, "*Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea wakabatizwa.*"

Wakateremka majini.

Mdo. 8:26-39, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake Malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, je yamekuelea haya unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule Towashi akamjibu Filipo, akasema, nakuomba nabii huyu anasema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake, akianza na andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji; tazama maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu, akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule Towashi; naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana*

akamnyakua Filipo, yule towashi asimuone tena; basi alikwenda zake akifurahi."

Maziko na ufufuo.

- Rum. 6:4, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hiivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"
- Kol. 2:12, "*Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo makfufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu.*"

Kupanda kutoka majini.

Marko 1:9-10, "*Ikawa siku zile Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho kama hua akishuka juu yake.*"

Unaona picha gani uanaposoma vifungu hivi? Kuna maji (maji mengi), wakateremka majini (maziko na ufufuo), na kupanda kutoka majini.

Vitu ambavyo umeona katika picha ya Mungu ya ubatizo.

Kiumbe kipya katika Kristo:

Maisha mapya.

Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu, kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

Tunafufuka kutoka katika kaburi la maji ya ubatizo katika uzima mpya.

Kielelezo kipya.

Kristo ndiye kielelezo cha Wakristo.

- 1 Pet. 2:21, "*Kwa sababu ndiyo mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake.*"

- Fil. 2:5, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.*"

Kama Wakristo tunapaswa kukumbuka kwamba yeye ni kielelezo chetu. Tunapaswa kujitahidi kuwa, na kujitahidi kuwaongoza wengine wawe Wakristo.

Tunapaswa kuangalia matendo yetu kwa "Kile ambacho Kristo angefanya?"

Mtazamo mpya.

Kiumbe kipya anapaswa kuwa na badiliko la moyo; kwa vile sasa anapenda haki, na kuchukia maovu.

- Rum. 12:9, "*Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema.*"
- Ebr. 1:9, "*Umependa haki umechukia maasi; kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, mafuta ya shangwe kupita wenzio.*"

Kusudi jipya.

Chochote ambacho mtu anakusudia katika maisha inaweza kuwa kabla, Mkristo hajawa na kusudi jipya.

Fil. 3:13, "*Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele,*"

Makusudi ya awali yanaweza kuishia katika ubinafsi, bali kusudi jipya ni kutumika.

Sasa inakuwa kubarikiwa kutoa kuliko kupokea.

Mji mpya.

- Yoh. 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu manamakao mengi kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"
- 2 Pet. 3:13, "*Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.*"

Kama mwanajeshi aliyeko pembeni mwa kambi ya moto, akifikiria nyumabni, akichukuliwa na usingizi na kuwaota wapendwa wake nyumbani; hivyo ndivyo askari wa msalaba anayefikiri vita anaaswa kukaza mwendo katika vita kwa mtazamo mzuri wa “mji ulioko pale.”

Hitimisho

Huwezi kudai ahadi hizi za ajabu kama wewe sio Mkristo.

Kama hujafanyika kiumbe kipya katika Kristo, kwa nini usifanye leo kwa utii wako rahisi kwa Kristo?

Juu ya imani yako ya kweli katika Yesu Kristo, tubu kwa ndani dhambi zako zote, na juu ya kukiri imai yako katika yeye, uzikwe pamoja naye katika ubatizo.

Alafu utafufuliwa ukiwa kiumbe kipya katika Kristo, “*utembee katika upya wa uzima.*”